

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI, 2014

MUDA: SAA 2 ½

## MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI WILAYA YA MAKINDU, 2014

*Hati ya kuhitimu elimu ya sekondari Kenya (K.C.S.E)*

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2 ½

### MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la kwanza ni la **lazima**.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani, Ushairi, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi simulizi.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka kwa sehemu moja.
- Karatasi hii ina kurasa tatu.  
Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## 1. USHAIRI (LAZIMA)

### Soma shairi hili kasha ujibu maswali

'Mepewa macho nione	nami sitayatumbuwa
Vikondefu na vinene	nipate kuvichunguwa
Pema na penye swenene	la kuwa na kutokuwa
Vipe nione mavune	nambie raha muruwa?
Nimepewa macho	sitayatofowa!
'Mepewa na sikiyo katu	sitolikwanyuwa
Ya kweli na singiziyo	nipate kuyabaguwa
Vipi sikie kemeyo	nite sauti ya hawa?
Bimadamu yake nia	tamu pate 'sikia
'Mepewa sikiyo	sitalibanduwa!
'mepewa na pua hino	kamwe sitaing' watuwa
Vioza pia vinono	puani kunukuliwa
Mnaso wake na vuno	na mnuko kuchenguwa
Vipi nisinuse pano	na kule kuna shuruwa?
Mepewa na puwa	sitaimeguwa!
'Mepewa huu ulimi	nami sitaunyotowa
Nitakalamu usemi	wenye nia na afuwa
Na maonjo vya vinyemi	sina budi kuchaguwa
Vipi nisionje kumi	na naoja nimecheuwa?
'mepewa ulimi	sitausokowa!
Nimepewa na hii ngozi	Katu sitaibanduwa
Hisia zinajalizi	zipate kusionuwa
Nyengine za maliwazi	nyengine za kubabuwa
Vipi nisihisi twezi	ngozi ikibabuliwa?
'Mepewa na ngozi	sitoichunuwa!
Nimepewa na nadhari	kupima na kupimuwa
Nende mwendo wa kadiri	wa kuhisi na kujuwa
Wa ku'zepuka hatari	zote zinokusudiwa
Vipi mimi nihiyari	hisia zangu kutwawa?
'Mepewa nadhari	sitoiondowa!

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)
- (b) Shairi hili ni la bahari gani? (alama2)
- (c) Eleza mtindo wa shairi hili (alama4)
- (d) Eleza ni kwa nini mshairi ametumia ritifaa katika shairi hili (alama2)
- (e) Eleza muundo wa shairi (alama 4)
- (f) Huku ukitoa mifano eleza vile mshairi alivyotumia uhuru wa kishairi (alama2)
- (g) Taja 'hisi' nne zilizotajwa na mshairi. (alama 2)
- (h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 3)
- (i) Swenene
- (ii) vioza
- (iii) Twezi

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

**Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea.**

2. Jadili nafasi ya vijana katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.  
au
3. Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.
- (i) Majazi
- (ii) Kinaya

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**Timothy M. Arege: Mstahiki Meya**

4. Tathmini mbinu alizotumia Mstahiki Meya kujiimarisha katika kiti cha utawala. (alama.20)  
Au
5. Eleza sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao. (alama 20)
- (a) Mstahiki Meya
- (b) Diwani wa III

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**Ken Walibora na Said A. Mohamed: Damu Nyeusi**

6. "Hapa huingii bila kuninyoshea mkono ....."
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Eleza sifa nne za mzungumziwa (alama 4)
- (c) Kwa kurejelea muktadha wa hadithi nzima thibitisha ukweli wa kauli kuwa mkono mtupu haulambwi. (alama 12)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

7. (a) Lakabu ni nini ? (alama 2)
- (b) Eleza sifa nne za lakabu (alama 8)
- (c) Eleza umuhimu wa lakabu (alama 10)